**Mradi wa Shughuli Wezeshi Ya Kuandaa Mpango-Kazi Wa Taifa Wa Udhibiti Wa Uchafuzi Wa Mazingira Ya Bahari (National Marine Litter Management Action Plan)**

## 1.0 Utangulizi

Plastiki ni bidhaa ambayo inatumika kwa kiasi kikubwa katika shughuli mbalimbali ikiwemo kutumika kama malighafi katika uzalishaji wa bidhaa zingine viwandani ikiwemo vifungashio. Hata hivyo, plastiki imegundulika kuchangia uchafuzi wa mazingira na kuleta madhara kwa afya na mazingira. Aidha, tafiti zimebaini kuwa kiasi kikubwa cha taka za plastiki huishia baharini ambapo zinaathiri mifumo-ikiolojia ya bahari ikiwemo vifo vya viumbe waishio baharini.

Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira Duniani (UNEP) wameandaa mradi kuhusu udhibiti wa uchafuzi wa mazingira ya bahari utokanao na taka za plastiki ambapo Tanzania ni moja ya wanufaika wa mradi huu.

Kwa sababu hiyo, Ofisi ya Makamu wa Rais inaratibu utekelezajiwa shughuli wezeshi ya kuandaa Mpango-kazi wa Taifa wa Kudhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari. Shughuli hii inafadhili wa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira Duniani (UNEP) kwa kushirikiana na Sekretarieit ya Mkataba wa Nairobi kuhusu Hifadhi ya Bahari. Thamani ya shughuli hii ni Dola za Marekani 110,000.00.

## 2.0 Lengo

Kuandaa Mpango-kazi wa Taifa wa kudhibiti uchafuzi wa mazingira ya baharini utokanao na shughuli zinazofanyika nchi kavu.

## 3.0 Eneo la Utekelezaji

Shughuli wezeshi hii ni ay Kitaifa huku eneo la kufanya majaribio likiwa ni katika Jijini la Tanga.

## 4.0 Shughuli zilizopangwa na Hali ya utekelezaji

a. Kufanya kikao cha wadau kwa ajili ya tathmini ya vyanzo vya uchafuzi wa mazingira ya Bahari nchini na kuandaa taarifa.

b. Kuandaa taarifa ya kina ya tathmini ya vyanzo vya uchafuzi wa mazingira ya Bahari nchini yenye mapendekezo ya mikakati ya kuandaa Mpango-kazi.

c. Kufanya kikao cha ngazi ya viongozi ili kuwasilisha matokeo ya tathmini iliyofanyika pamoja na rasimu ya Mpango-kazi.

d. Kufanya vikao vya wadau ikiwemo sekta binafsi kwa ajili ya kuboresha na kukamilisha rasimu ya Mpango-kazi utakaoandaliwa.

e. Kufanya kampeni ya uhamasishaji kwa wananchi wa eneo la utekelezaji wa shughuli husika (Jijini Tanga).

f. Kufanya majaribio ya Mpango-kazi katika eneo la utekelezaji wa shughuli.